265. TU wasafiri

265

1. Tu wasafiri, twakaribia nchi ya mbingu kwa Mungu baba. Tusiogope bonde la kufa, Yesu atuongoza kwake!

Pambio:
:/: Tu wasafiri:/: tutakutana nyumbani mwa Baba. E' Bwana Yesu utuongoze, tufike sote mbinguni!

2. Wengi katika wapendwa wetu wamevuka mto wa kufa. Walifuata mwito wa Mungu. Wakahamia nchi nzuri.

3. Katika mwendo wa duniani walitazama Mwokozi wao, na waliacha mambo ya huku, walipendeza Bwana Yesu.

4. Ndugu wapendwa, tuendelee, hata ikiwa shida njiani! Yesu ni njia, kweli, uzima; tumfuate siku zote! Paul Ongman